



# TAARIFA HALISI NAMBA TATU



## “TATHMINI ZAIDI NI MUHIMU KATIKA MABADILIKO YA TABIA”

Shughuli mbalimbali zinazofanyika kuhusu kinga hulenga katika kuhuisha zile tabia hatarishi katika maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Katika nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, shughuli hizi zinalenga katika kupunguza tabia zifuatazo:-

- Kufanya ngono bila kinga
- Kufanya ngono na wapenzi wengi kwa kipindi kimoja
- Kuanza kufanya ngono katika umri mdogo
- Kufanya ngono na watu walio katika hatari zaidi.

Kubadili tabia siyo kazi rahisi: Hata hivyo, yapo mafanikio machache yaliyopatikana katika jitihada za kuhamasisha mabadiliko ya tabia. Kwa mfano mwaka 2005, kiwango cha maambukizi kilishuka nchini Kenya na Zimbabwe ambapo matumizi ya kondomu yaliongezeka, kuchelewa kujiingiza katika mapenzi na kutokuwa na wapenzi wengi kulichangia kwa kiasi kikubwa kupunguza kwa kiwango hicho cha maambukizi, (utafiti wa UNAIDS). Zipo pia dalili za mabadiliko ya tabia nchini Swaziland na Afrika Kusini.

- Nchini Kenya, matumizi ya kondom kwa wapenzi wasio wa kudumu yaliongezeka hasa miongoni mwa wanawake; mwaka 2003, asilimia 24 ya wanawake walitumia kondomu ikilinganishwa na asilimia 15 mwaka 1998. Aidha, uwiano wa wanaume na wanawake wenye mpenzi zaidi ya mmoja ulipungua kwa zaidi ya nusu kati ya mwaka 1993 na 2003. Utafiti uliofanyika mwaka 2004 unaonyesha pia kwamba vijana wengi hawakujiingiza katika vitendo vya ngono mapema na viwango vya maambukizi ya magonjwa ya ngono vilipungua.
- Nchini Zimbabwe, kiwango cha maambukizi ya virusi vya UKIMWI miongoni mwa vijana walio kati ya umri wa miaka 15 na 24 kilipungua kutoka asilimia 29 hadi asilimia 20 kati ya mwaka 2000 na 2004. kiwango hicho kiliweza kushuka kutokana na watu wengi kuitikia matumizi ya kondomu na kupunguza idadi ya wapenzi.
- Huko Swaziland kiwango cha maambukizi kilishuka kwa asilimia nne miongoni mwa wasichana wadogo jambo ambalo Waziri wa Afya wa nchi hiyo alilichukulia kwamba **“Ujumbe kuhusu kuzuia maambukizi umeeleweka”**
- Hali Kadhalika, nchini Afrika Kusini, matumizi ya kondomu na kupunguza idadi ya wapenzi viliweza kupunguza kiwango cha maambukizi mwaka 2005.

**Hapa Tanzania matumizi ya kondomu yameongezeka kutoka chini ya kondomu milioni moja (<1,000,000) kwa mwaka, mwishoni mwa miaka ya 1990, na kufikia karibu kondomu milioni miambili (200,000,000) hivi sasa.**



# TAARIFA HALISI NAMBA TATU



**Kulingana na matokeo ya Utafiti wa Afya na Idadi ya watu ya 2004/05 hapa nchini, matumizi ya kondomu kwa makundi yaliyo katika hatari zaidi ya maambukizi – yaani vijana wenye umri wa kati ya miaka 15 na 24, yalifikia asilimia 37 kwa wasichana na asilimia 46 kwa wavulana.**

Mikakati mikuu iliyopo katika hamasa za mabadiliko ya tabia ni pamoja na kampeni za Mawasiliano, Elimu juu ya UKIMWI na Stadi za maisha, elimu kwa vijana walio nje ya shule na makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kuambukizwa pamoja na usambazaji wa kondomu.

Mafanikio au kutofanikiwa kwa mikakati iliyotajwa kunaweza kupimwa kwa kuangalia kiwango cha maambukizi miongoni mwa makundi ya vijana. Iwapo kiwango cha maambukizi kinaongezeka ni dhahiri kwamba mikakati hiyo haikufanikiwa. Hata hivyo, mara nyingi masuala ya mabadiliko ya tabia yanafanyika kwa makundi machache hivyo matokeo yake yanaweza yalitambulike katika kiwango cha kitaifa.

## Majumuisho

Mafanikio ya kampeni za kubadili tabia yanategemea utayarishaji wa taarifa zilizo sahihi na kuhakikisha kuwa zile huduma ambazo watu wanahitaji ili waweze kubadili tabia kama vile kondomu na ushauri nasaha zinapatikana kwa urahisi.